

**TAARIFA FUPI YA ZAHANATI YA KIJIKI MAGANAGANA, KWA
KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA NDUGU,
CHARLES FRANCIS KABEHO TAREHE 05-06-2018**

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Ninayo furaha kubwa sana kukukaribisha wewe pamoja na msafara wote uliofuatana nao hapa katika Zahanati ya kijiji Maganagana, nasema karibu sana na ujisikie upo nyumbani.

Ndugu, Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Zahanati ya Kijiji cha Maganagana ilianza kujengwa mwaka 2015 na imekamilika mwaka huu 2018

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Ujenzi wa mradi huu wa Zahanati hadi kufikia sasa imegharimu kiasi cha tshs **41,628,600/=**, **Kati ya** fedha hizo nguvu za Wananchi Tshs **20,787,600/=**, mchango wa Halmashauri kupitia mapato yake ya ndani Tshs **20,091,000/=** na mchango kutoka mfuko wa Jimbo ni Tshs **750,000/=**

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Zahanati hii imejengwa kuepukana na adha ya Wananchi kutembea umbali mrefu kufuata huduma hii muhimu ya afya, Pia itasaidia kupunguza idadi ya vifo vya Mama wajawazito na Watoto walio chini ya Miaka Mitano . Zahanati hii itanufaisha Jumla ya Wananchi 1600 Walipo katika Kijiji hiki.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Huduma zitakazo tolewa katika Zahanati hii ni; huduma za wagonjwa wa nje (OPD), huduma za wagonjwa wa ndani (In Patients), huduma za meno, huduma za Mama na Mtoto na pia upasuaji mdogo utafanyika.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Zahanati hii itasaidia kuboresha Afya kwa Wananchi ikiwa ni pamoja na Wanafunzi kwa maana ya kwamba Wanafunzi Wakiwa na afya bora wataweza kumudu masomo vizuri hivyo kuwa na Jamii iliyoelimika ambayo italeti maendeleo ya Kiuchumi na kijamii katika Kijiji chetu. Kwa umoja wetu tunaunga mkono kaulimbiu inayosema **‘Elimu ni ufungu wa Maisha; Wekeza sasa kwa maendeleo ya Taifa letu’**

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Baada ya taarifa hii, kwa heshima na taadhima, sasa nakuomba ufungue rasmi Zahanati ya kijiji Maganagana.

Ni mimi,

Musa Madamba
AFISA MTENDAJI KIJJI
KWA NIABA YA WANANCHI KIJJI CHA MAGANAGANA